

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**



**TAARIFA RASMI YA USAFIRI (TRAVEL ADVISORY)**

**Dodoma, Novemba 04, 2025**

Wizara ya Maliasili na Utalii inapenda kuufahamisha umma, wageni na wadau wa Sekta ya Utalii ndani na nje ya nchi, kwamba hali ya amani na utulivu imerejea na shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi zinaendelea baada ya kudhibitiwa kwa vurugu zilizoibuka kati ya tarehe 29 Oktoba hadi 1 Novemba, 2025. Kwa msingi huo tunawataarifu kwamba:

Tanzania kama Mwanachama wa Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism), inatekeleza na kusimamia Mwongozo wa Utalii Kimataifa unaoelekeza nchi kuhakikisha usalama wa wageni, ikiwemo wasafiri na watalii wanaotembelea maeneo mbalimbali wawapo nchini.

Vituo vyote vya kuingia na kutoka nchini kupitia usafiri wa anga, barabara, maji, reli, sambamba na usafiri wa umma vinaendelea kutoa huduma kwa utaratibu wa kawaida. Aidha, shughuli za utalii na huduma kwa wageni zinaendelea kutolewa katika maeneo yote nchini kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Wasafiri wanahimizwa kuendelea na mipango yao ya kutembelea na kufurahia vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo Tanzania bila hofu yoyote.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuwa nchi salama, yenye utulivu, na mazingira rafiki kwa shughuli zote za usafiri, uwekezaji kibiashara na utalii; hivyo, Serikali inachukua fursa hii kuwakaribisha wageni wote nchini.

Imetolewa na;

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Nteghenjwa Hosseah'.

**Nteghenjwa Hosseah  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM**



**OFFICIAL TRAVEL ADVISORY**

**Dodoma, 04<sup>th</sup> November, 2025**

The Ministry of Natural Resources and Tourism wishes to inform the public, visitors, and tourism stakeholders that peace and stability have been fully restored throughout the United Republic of Tanzania. All social, economic, and tourism activities are proceeding normally following the swift containment of recent post-election incidents.

As a committed Member of the United Nations Tourism Organization (UN Tourism), Tanzania upholds international standards ensuring the safety and well-being of all travelers. All entry and exit points — by air, land, sea, and rail — remain fully operational, and tourism services across the country continue without disruption.

Travelers are therefore encouraged to proceed with their plans to visit and explore Tanzania's exceptional attractions with confidence. The United Republic of Tanzania remains a peaceful, stable and welcoming destination for tourism, business and investment.

Issued by

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Nteghenjwa Hosseah'.

**Nteghenjwa Hosseah**  
**Head of Government Communication Unit**